



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



**RATIBA YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI**  
**(PRIMARY SCHOOL LEAVING EXAMINATION TIMETABLE)**  
**SEPTEMBER, 2023**

TAREHE NA SIKU	MUDA (SAA)	NAMBA MFICHO	SOMO
<b>13.09.2023</b> <b>JUMATANO</b>	2:00 – 3:40	01	KISWAHILI
	<b>3:40 – 4:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	4:30 – 6:30	04 04E	HISABATI MATHEMATICS
	<b>6:30 – 8:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	8:30 – 10:00	05 05E	SAYANSI NA TEKNOLOJIA SCIENCE AND TECHNOLOGY
<hr/>			
<b>14.09.2023</b> <b>ALHAMISI</b>	2:00 – 3:40	02	ENGLISH LANGUAGE
	<b>3:40 – 4:30</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	4:30 – 6:00	06 06E	URAI NA MAADILI CIVIC AND MORAL EDUCATION
	<b>6:00 – 8:00</b>		<b>MAPUMZIKO</b>
	8:00 – 9:30	03 03E	MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI SOCIAL STUDIES AND VOCATIONAL SKILLS

## MAELEKEZO MUHIMU

1. Hakikisha kuwa unayo **Ratiba ya Mtihani ya mwaka 2023** iliyoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.
2. **Kabla ya kufungua bahasha** yoyote yenye maswali ya mtihani, hakikisha kwamba **unasoma jina la somo juu ya bahasha husika** na kujihakikishia kuwa somo hilo ndilo linalostahili kufanyika wakati huo kulingana na **Ratiba ya Mtihani**.
3. Endapo utata utajitokeza kati ya **maelekezo yaliyomo katika Karatasi ya Mtihani na Ratiba ya Mtihani, maelekezo yaliyomo katika karatasi ya Mtihani husika ndiyo yatakayofuatwa.**
4. Watahiniwa wenye mahitaji Maalum (**Wasioona, Uoni hafifu, Viziwi**) waongezewe **MUDA WA ZIADA WA DAKIKA 20 KWA KILA SAA** kwa somo la **Hisabati na DAKIKA 10 KWA KILA SAA** kwa masomo mengine.
5. Msimamizi wa watahiniwa **wenye mahitaji maalum** awe **Mtaalamu** mwaminifu wa mahitaji **husika**.
6. Watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** wapewe karatasi za mtihani na za kujibia zenye **maandishi yaliyokuzwa**, zilizoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa matumizi yao.
7. Karatasi zenye majibu ya watahiniwa wenye **UONI HAFIFU** zifungwe kwenye **bahasha za pekee**. Zisichanganywe na karatasi za watahiniwa wenye Uoni wa kawaida.
8. Watahiniwa waelekezwe;
  - (a) Kuingia ndani ya chumba cha Mtihani nusu saa kabla ya muda wa Mtihani na watakaochelewa kwa zaidi ya nusu saa baada ya Mtihani kuanza hawataruhusiwa.
  - (b) Kufuata maelekezo yote yatakayotolewa na wasimamizi wa Mtihani.
  - (c) Kuandika namba ya Mtihani kwa usahihi.
  - (d) Kuhakikisha namba iliyoandikwa kwenye msimbomilia na namba ya Mtihani zinafanana.
  - (e) Kutofanya mawasiliano ya maneno au kwa njia yoyote baina ya watahiniwa. Ikiwa mtahiniwa ana tatizo anatakiwa kunyoosha mkono ili kuomba msaada kwa msimamizi wa Mtihani.
  - (f) Watakaojihusisha au watakaofanya udanganyifu watafutiwa matokeo yao ya Mtihani.